# Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Familia

tarehe 15 mwezi wa 5, 2010

Kunduchi, Dar es Salaam, Tanzania



## *Karibuni*

Ninafurahi sana kufungua sherehe ya kimataifa ya familia katika mkusanyiko huu. Hii si mara ya kwanza kuwa pamoja tarehe 15 Mei : Tulikwisha sherehekea siku hii mwaka 2005, 2006 na wengi wenu huenda wanakumbuka kuwa tuliitumia siku nzuri ya Mei 15 ukumbi wa baa ya Mwananyamala Garden.

## Tunatoka maeneo mbalimbali

Kama kawaida tunatoka maeneo tofauti tofauti na yanayoizunguka ***Dar es Salaam***. Baadhi yetu wanatokea kwenye ***machimbo ya Kunduchi*** ambapo tupo leo hii na pia kutoka ***machimbo ya Boko na Tegeta***, wengine wanatokea ***Soko la samaki la Magogoni***, wengine kutoka ***Tandale*** na hata majirani wa Dar es Salaam.



Na mwaka huu tuna nafasi ya kuwakaribisha washiriki kutoka mbali. Kwanza, Jules, Emile na Justin kutoka ***Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo*** kwa ajili ya kusherehekea nasi siku hii. Watatutolea ushahidi wa kujitoa kwa watu wa Kongo katika vita dhidi ya umasikini uliokithiri.



Pili, tunawakaribisha Jean na Fabienne ambao ni ***wawakilishi wa ATD Dunia ya Nne kwa Afrika*** na ambao mara nyingi wanaishi na kufanya kazi Bangui katika Jamhuri ya Afika ya kati.

## Sisi ni wajumbe na Marafiki wa harakati hizi ATD Dunia ya Nne

Sisi sote tunakataa ubaya wa umasikini uliokithiri. Sisi sote tunakataa, baadhi ya watu kutokuchukuliwa kama wanadamu. Sisi sote tunashawishika kuwa “watu wote wanathamini ya asili ambayo husimamisha heshima ya utu wao. Sisi ni wajumbe na marafiki wa harakati sawa ATD Dunia ya Nne. ATD inamaanisha “Sote pamoja katika utu”.

## Leo ni siku ya kimataifa ya familia

Leo, Mei 15 ni siku ya kimataifa ya familia. Siku hii ilisherehekewa tangu mwaka 1994 katika nchi nyingi zaidi na zaidi. Ili vumbuliwa na Umoja wa mataifa kwa ajili ya kuzikumbusha nchi umuhimu wa kusaidia familia na kuzipa kipaumbele katika maamuzi ya serikali.

Sherehe hii kama tuifanyavyo hii leo ni muhimu kwa sababu inaonyesha kuwa familia zimehamasika kwa ajili ya kubadilisha maisha ya baadaye ya watoto wao.

## Sisi ni wanaharakati kuupinga umasikini uliokithiri : Kwanini tunasherehekea siku hii ?

Kama unavyojua, ATD Dunia ya Nne hulenga kuushinda umasikini uliokithiri. Ni kiunganishi kipi kilichopo na familia hizo ?

Watu wote wanaoishi katika hali ngumu husema kuwa ni familia zao ambazo huwapa nguvu kustahimili siku baada ya siku. Joseph Wresinski, muasisi wa ATD alisema kuwa “familia ni ngao inayozuiya uharibifu wa umasikini uliokithiri kwa binadamu”. Ndio maana, kupitia siku hii, tunataka kusherehekea na kuzipa heshima familia zote.

## Watoto wa mtaani wa Ouagadougou (Burkina Faso) wanasema nini kuhusu familia zao ?

Februari iliyopita Salehe alikuwa Burkina Faso na alishiriki katika maktaba ya mtaa. Unajua nini, kila jumatano kuna maktaba ya mtaa kwa majirani zako wa Tandale. Hata hivyo huko Burkina Faso, maktaba ya mtaa hufanyika usiku panapokuwa kiza na panapokuwa hakuna mtu tena katika mitaa isipokuwa watoto wa mitaani.

Kwa sababu kadhaa, watoto hutengana na familia zao, lakini hawazisahau. Wanasema nini kuhusu familia zao ? Haya ni baadhi ya wanayoyasema.



> *“Tungalipenda kuwa na maisha bora. Maisha ambayo ni kuwa na nyumba, kuweza kuamka asubuhi na kwenda kazini. Maisha ambayo ni kuwa na mke na familia. Maisha yetu haya, hayatatupatia lolote katika maisha yetu ya badaye. Sisi ambao tunaishi mitaani hatuheshimiwi hata na wadogo zetu. Kama utapata kazi, utaheshimiwa, maisha ni kama hivi.*
>
> *Ili kukuwa vyema, tunahitaji sana kutiwa moyo. Kufikiria kuhusu familia zetu hutupa moyo. (...) Ili tufanikiwe katika maisha yetu, tunatakiwa kuwa waadilifu, waaminifu na kutovunja heshima ya familia zetu. Tunatakiwa kufikiri kwa njia nzuri, hii ni kuwa mtu anaetaka kuwa ni manufaa kwa wengine. (...)*
>
> *Pindi mmoja wa ndugu zetu anapofariki, kama hatuko kijijini hatuwezi kujua. (...)*
>
> *Msamaha ni muhimu kwa sababu bila kusameheana huwezi kukaa katika familia yenu. Haiwezekani kukataa msamehe.”*

## Shughuli ya leo




Kabla ya kuwapa ratiba ya siku hii ambayo tutasherehekea (tutaitumia) pamoja, tutasoma shairi dogo lililoandikwa na watoto kutoka Cameroon ili kutukumbusha kuwa leo ***duniani kote*** watu wengi sana hukusanyika kama tulivyofanya kwa ajili ya kusherehekea siku ya kimataifa ya familia.

***Kutoka Yaounde***, mji mkuu wa Cameroon, ***tumepokea shairi*** hili lililoandikwa na watoto kuhusu maana ya umaskini kwao. Kwa mara nyingine wanaelezea kivipi familia zao ni muhimu kwao katika kuupinga umasikini.




*Umasikini ni pale watu wanapokosa chochote kitu ili kuishi maisha yenye heshima,*
*Umasikini ni pale dada yangu mdogo anapoumwa,*
*Umasikini ni pale ambapo watu wanataabika,*
*Umasikini ni pale ambapo baba yangu anapokuwa hana kazi na bila ya fedha yoyote,*
*Umasikini ni pale tunaposhindwa kwenda shule,*
*Umasikini ni wakati panapokuwa na vita,*
*Umasikini ni pale tunapokuwa hatuna chakula,*
*Umasikini ni pale ambapo huwa bila familia,*
*Umasikini ni pale ambapo watoto hulazimika kutafuta chakula jalalani,*
*Umasikini ni pale tunapokosa makazi.*

## Shughuli za kufanya



Sasa tunakwenda kuona shughuli za leo. Kwa kweli shughuli hizi zitakuwa ni za kufurahisha na kuvutia sambamba na muziki na kucheza wakati fulani.

## Tutasikiliza shuhuda na maelezo kuhusa “kujitoa”

Sehemu ya kwanza ya mkusanyiko wetu itakuwa ni kujitoa. Sisi sote tunataka maisha ya baadaye yaliyo mazuri kwa watoto wetu na familia zetu. Tunataka watoto wetu waweze kwenda shule, tunataka watoto wetu kuweza kupata huduma za afya, tunataka watoto wetu waweze kushiriki kikamilifu katika kujenga jamii tulivu ambayo kila mtu atakuwa akiheshimiwa. Baadhi yetu wapo tayari kujihusisha wenyewe katika njia tofauti tofauti. Tutasikiliza ujumbe na shuhuda zao.

Kisha tutasoma maelezo kuhusu “kujitoa” kwa watu wanaoishi katika hali ngumu na tutashiriki kutoa maoni na mitazamo yetu.

## Kwa pamoja, tunaongoza miradi halisia

Katika sehemu ya pili, baadhi yetu wataeleza ni miradi ipi ambayo tumeianza katika maeneo yao kupitia vikundi vyao. Tutaona kivipi inawezekana kwa wengine kuanza miradi hiyo katika maeneo yao.

## Hitimisho pamoja na watoto na chakula cha mchana.

Kwa kumalizia na kabla ya kupata chakula cha mchana kwa pamoja, watoto watajumuika nasi na watashirikinasi walichokifanya wakati wa mkutano wetu.





## *Shuhuda*

Tunakwenda kusikiliza baadhi ya shuhuda toka kwa watu mbalimbali ambao wamejitolea maisha yao ya kila siku katika kupambana na umasikini uliokithiri. Kama tunavyojua, kama tunataka kuushinda umasikini uliokithiri, haitoshi kuomba na kusubiri wengine wafanye. Kila mmoja wetu anatakiwa kusimama na kutenda. Wengi wetu tayari wanachukua hatua, hapa Tanzania na mahali pengine duniani. Kwa kweli ni faraja kwa kila mtu kujua kuwa hayuko peke yake katika mpambano huu na ndio maana, ni muhimu kushirikishana ujuzi wetu.

## Umoja waleta nguvu

(shuhuda ulisomwa na Jules BACHIRONGO BAHATI)




Wakati inchi yetu ya Jamhuri ya Kidemokratia ya Congo ina ndoto ya kuwa na amani na starehe, bado usalama mdogo unaripotiwa hapa na pale vijijini. Hali hiyo inawapeleka watu kuyakimbia makao na vijiji vyao na kutafuta mahali penyi amani.

Kijiji changu cha Bitale/Bunyakiri ni mmoja wa hivyo vijiji vinavyo sumbuliwa na wamiliki silaha kwa kuwatesa raiya, kupora mali, kuwabaka wa binti na wa mama zetu, kuwauwa watu wamoja wamoja na hata wengine kupelekwa porini na wajambazi hao.

Jamaa yangu nimmoja ya wahanga wa hali hiyo ya ujeuri. Tulipokimbia tulikaribishwa na babu mmoja aliye kuwa na nyumba ndogo saana. Kiisha kuchunguza hali hiyo ya msongamano katika nyumba hiyo ndogo, tuliamuwa kujenga ingine nyumba. Kwa msaada wa watu wa moyo mwema, vijana kama mimi hata watoto, nyumba hiyo imejengwa muda wa siku chache. Kila mtu alipana mchango wake kadiri awezavyo. Wamoja walitolea vifaa vya ujenzi kama vile miti, matete, kamba, nyasi... na wengine walishiriki kwa kujenga. Mpaka sasa mimi na jamaa langu tunaishi ukimbizini katika nyumba ambano hakuna tena msongamano wa watu. Ijapo umaskini watu wa moyo mwema wanatualika shambani mwao kuvuna chakula. Baba yangu, kiisha kuguswa na kitendo hiki cha mapendo alisema *“kweli umoja kati ya watu huleta nguvu kwani tulikuwa bila makao kamili ila muda wa siku chache tumepata nyumba”*.



## Jamii yetu inahusika kabisa kusaidia familia hii

(ushuhuda wa Mama Niko ulisomwa na Mama Soni)

Naitwa Mama Niko, ninaishi Tandale. Nitawaeleza jinsi Mimi na Majirani zangu tunavyo msaidia mwenzetu.

Wiki kadhaa zilizopita mwenzetu huyo alikuwa ni mgonjwa sana na aliyedhoofika, alikwenda mara kadhaa hospitali na kufanya vipimo mbalimbali kama typhoid, X-ray ya kifua, nk.

Ilibidi tujadili na kupigania ili haki ya mgonjwa wetu ya kupata huduma iheshimiwe. Kila mara alikuwa ni kama mtu aliye changanyikiwa na kutokana na hali hiyo ilimpelekea kutokufuatilia matibabu kikamilifu na hali kuwa mbaya zaidi. Hapo ndipo Mimi, majirani wenzangu na Mumewe tulipoamua kumrudisha hospitali kwa uangalizi zaidi. Huko hospitali, baada ya kulipia kibajaj maji ya kunywa ya mgonjwa pamoja na malipo ya uandikishaji wa kadi la mgonjwa, hatukuwa na fedha yoyote kwa ajili ya kulipia kumuona daktari. Hapo ndipo wakakataa kumpokea na kumpa kitanda mgonjwa wetu.

Niliporudi nyumbani, niliwakuta majirani wenzangu ambao walianza kupika chakula kwa ajili ya mgonjwa wetu. Tangu hapo kila siku tuliandaa chakula na haikutuwia vigumu kuandaa kwani mgonjwa wetu hakuwa mchaguzi wa chakula. Wakati mwingine mimi pamoja na majirani wenzangu huchangisha fedha kwa ajili ya kumuandalia chakula anachokipenda maji na nauli kwa anaempelekea.




Hata mumewa wakati mwingine humpelekea chakula, na pia mgonjwa hula sana anapokuwepo mumewe.

Mtoto wake wa kike hulala nyumbani na wanangu na huwa ninamfulia nguo zake pia, hukaribishwa chakula na majirani wote lakini, sasa amesimama kwenda shule kwa sababu amepoteza madaftari yake.

Huwa tunamtembelea mara kwa mara, wawili kati yetu humtembelea kila siku na ni faraja kwake kujua kuwa familia yake haijatengwa.

Ni muhimu sana kwetu kumsaidia mwenzetu na familia yake. Kila jirani yuko tayari kuchangia au kusaidia kwa njia moja au nyingine kulingana na uwezo alionao. Jirani mmoja hutoa Chapati mbili kila siku kwa mtoto wa mgonjwa, baadhi huchangia fedha, wengine humtembelea hospitalini kumfariji, wengi huchangia gharama za maji au usafiri. Jamii yetu inahusika kabisa kusaidia familia hii.

## Watoto wanayo mengi ya kuwafunza wakubwa

(shuhuda ulisomwa na Justin BYAMUNGU MBALE)




Pa Bukavu kuna jamaa ya mtoto mmoja apatikanaye katika kikundi cha watoto Tapori na aitwaye kwa jina la Destin. Myezi iliyopita, hiyo jamaa ilipatwa na shida kali saana kwani nyumba, mali na vitu vyote vimeunguzwa na moto. Kwa bahati nzuri hakukuripotiwa vifo vya watu sababu kitendo hiki kimepitika mchana kati. Kwa muda wa siku chache, jamaa hiyo imekaribishwa na ingine jamaa jirani. Hizo tukio za kuunguzwa kwa nyumba na vitu vyote ilishurutisha Destin na jamaa lake kuishi katika hali ya umaskini kabisa kwani wazazi hawana kazi nzuri iliwapate kuhudumia jamaa nzima. Hali hiyo ya uchungu iliwagusa watoto wengine wenye wanashiriki na Destin katika kikundi ya watoto Tapori. Hawa watoto walikusudia kwenda kumupongeza rafiki yao Destin na jamaa lake. Wiki moja mbele ahadi hiyo itimizwe, kila moja wa hawa watoto alienda kujulisha habari hiyo ya uchungu kwa wazazi wake. Wazazi waliguswa na hali hiyo, walitolea zawadi mbalimbali kama vile mabuku, kalamu, sabuni, mavazi, pesa, yote kwa ajili ya jamaa ya Destin. Na huko, watoto walifanya mkutano wao wa Tapori, walichapa sanamu, waliimba, walitolea ujumbe mbalimbali wa pongera na walitolea pia zawadi walizopewa na wazazi kwa jamaa ya Destin. Alipoguswa saana na hiki kitendo nzuri cha watoto wa Tapori, mama mzazi wa Destin aliwatolea watoto ujumbe huu:”kweli nyinyi watoto munayo mengi ya kutufunza sisi wakubwa kwa sababu munakuwa wa kwanza kuguswa na shida iliyopatwa na jamaa langu. Muendelee vile sababu ulimwengu wa kesho unahitaji upendo, urafiki na juhudi kama yenu”.



Kiisha wiki moja, kupitia huo mfano wa watoto wa Tapori, wakubwa wamoja wamoja nao walienda kupongeza jamaa la Destin na kutolea kila mtu kadiri awezavyo (urafiki, kicheko, chakula, sabuni na vivi hivi).

## Kazi ya pamoja, husaidia zaidi

(ushuhuda alisomwa na Emile HABAMUNGU CHIRHANACHO)



Katika kikundi chetu cha "jamaa ushirika la Burhiba/Bukavu" kuna baba moja aitwaye kwa jina la MULAMBA ISIDORE. Yeye anafanya kazi ya kubeba mizigo kwenyi beach Muhanzi/Bukavu. Wakati vyombo vya majini vinakuja na pombe za asili inayoitwa kasiksi kutoka vijijini, kazi yake nikutosha pombe kwenye chombo na kuibeba sokoni. Chombo hiki kinazoweya kubeba jerekani za pombe miya tatu (300) ya litri ishirini (20). Akiisha kupakuwa na kubeba jerekani hizo za pombe mchana mzima pamoja na wenziye: magaribi wanakusanya pesa walio pata na kuigawa kati yao. Kazi hiyo wanaifanya katika kikundi kwasababu mtu moja hawezi weza kupakuwa na kubeba jerekani hizo zote. Wakiisha gawa pesa, kila mtu anaweza kupata dola tatu (3$) kwa siku. Kwa pesa hizo, bwana MULAMBA ISIDORE anatosha dola mbili nakumupa mke we kwa kutafuta chakula kwaajili ya jamaa na dola moja anipana katika kikundi kwaajili ya mchango (likilimba) mara mbili katika wiki. Mchango huo unasaidia kila mwanamemba wao kueneza pesa kwaajili ya kulipa shule kwa watoto, kwani kiisha mwezi mmoja, kila mtu hupata dola ishirini (20$). Na hizo pesa husaidia jamaa la bwana MULAMBA ISIDORE kulipa shule kwa vijana wao wawili wenye kusoma katika shule ya segondari. Pia, pesa hizo za mchango ilisaidia jamaa hiyo kupata ufugo ; hadi leo wanahesabu mbuzi tano na nguruwe moja. Na huo ufugo, wakati unaongezeka, unasaidia pia katika shida zingine nyumbani. Na pia, huo mchango (likilimba) unasaidia bwana MULAMBA kuishi urafiki, undugu, umoja na wenziye.

## Kukosa usingizi kwa mapendo ya jamaa

(ushuhuda ulisomwa na Emile HABAMUNGU CHIRHANACHO)




Katika kata langu, kuna mtu moja aitwaye kwa jina la MWEZE Julien. Bwana huyo hufanya kazi ya uvuvi wa samaki tangu myaka mingi. Kazi hiyo, anaifanya kwenyi ziwa kivu/Bukavu kila siku usiku. Katika mwezi, analala nyumbani mara tatu ao mara nne tu. Wakati wa hasubuyi, samaki alizo pata anazipa mkewe azitwae sokoni. Mehana Bwana MWEZE hufanya kazi yakutengeneza wavu wake ili apate tena kuvua samaki usiku. Mara nyingi hapati muda wakupumuzika. Yeye na mkewe wana watoto saba (7) na kati yao watano wanaenda shuleni. Napesa ipatikanayo wakati mkewe anauza samaki sokoni ndiyo inasaidia nyumbani kwa kulipa shule kwa watoto na kuhudumia shida zingine za jamaa. Ila si raisi kwa jamaa hiyo kulipa kila mwezi shuleni dola ishirini (20). Lakini baba huyu, anasema mara na mara kama anawalipia watoto pesa hizo kwani anafahamu kama shule ni ya muhimu sana maishani mwa mwadamu ; mtu asiye elimishwa hupatwa na magumu mengi maishani mwake.

Wakati wakubwa wa nchi wanafunga uvuvi ndani ya ziwa kivu, ndipo maisha yanakuwa magumu zaidi kwa jamaa hiyo. Hapo baba na mama hufanya kazi ya kubeba mizigo ili watoto wasikose hata chakula kwani hizo pesa haziwezi kulipa shule kwa watoto.







**Wakati wazazi wanabadilishana mawazo na uzoefu, Mwalimu Laswai na baadhi ya vijana wa ATD Dunia ya Nne : Kitwana, Amina, Bibiye, Peter na Karama wakicheza, wakichora, wakisoma hadithi mbalimbali na kuimba pamoja na watoto.**









## *Tutasoma maelezo yaliyoandikwa na Joseph Wresinski*

Sasa tutasoma maelezo yaliyoandikwa na Joseph Wresinski ambaye ni muasisi wa Harakati za kimataifa za ATD Dunia ya Nne. Aliandika maelezo haya zaidi ya miaka 30 iliyopita ili kuiuliza jamii ya kifaransa kuhusu utayari wake katika kuutokomeza umasikini uliokithiri.

Shauri lake, lilihutubiwa kwa wahusika mbalimbali wa jamii : viongozi wa siasa, wananchi wanaojiweza, wanahiyari wa kudumu wa ATD Dunia ya Nne na familia zilizo katika hali ngumu sana.

Tunakwenda kusikiliza maelezo hayo isipokuwa sehemu ya mwisho, ilihutubiwa kwa familia ambazo hupigana kila siku dhidi ya umasikini kama wengi wetu tuliopo hapa.

Kisha tutakuwa na muda wa kushiriki pamoja mawazo yetu.

## Joseph Wresinski – Paris – tarehe 17 Novemba 1977

*(…) Nawasihi, familia zinazoishi katika mazingira magumu.*

*Ni kukataa kwenu kuishi bila matumaini, ni kukataa kwenu kudhaniwa kuwa ni wenye dhamana ya tabu mnazo zipata na pia kufanywa kama hamkuwahi kuwapo au kama msio na faida yoyote, ni kitu ambacho kimetia moyo harakati zetu. Harakati zetu si chochote kama si kuonyesha kwenu kuchukizwa na pia kiliochenu kuhitaji msaada.*

*Hata hivyo, mnajua kuwa hakuna mtu atakae wafanya muwehuru bila ya juhudi zenu. Mmekuwa mkiangushwa mara nyingi sana. Mnajua kuwa jamii nyingine hazina mawazo wala moyo wa kutaka kujua kama ninyi au hata kuwa na mipango kama yenu. Hii ndio maana ninyi ni wakwanza kuwajibika kwa mabadiliko ya maisha yenu, mtakuwa wa kwanza kubeba mzigo.*

*Na ili kuweza kuwajibika, kwanza utaendelea na mafunzo, kujifunza na kukusanyika kwa ajili ya kufikiri kuhusu hali mliyonayo (...) Tutalenga (...) kufuta ujinga, kuboresha mahudhurio shuleni na kuwahakikishia mafanikio ya watoto shuleni.*

*Tunahitaji msaada wa wengine kufanikisha malengo haya, lakini pia tutashiriki kwa sehemu yetu bila wasiwasi. Waache wale wanaojua kusoma na kuandika wawafundishe majirani zao. Hebu tuwatie moyo vijana wetu kuhudhuria mafunzo ya ufundi. Acha kila mmoja wetu awajibike kwa mafunzo yetu ya ufundi na kuwajibika kwa wengine pia.*

*Kuwajibika pia ni kuunganisha familia katika jumuiya mbalimbali, jumuiya za wazazi na walimu, jumuiya za wafanyakazi, umoja wa wafanyabiashara na vyama vya siasa. Wewe pia una haki ya kupigania uadilifu, amani na haki za binadam. Kuwajibika ni kushiriki katika mapambano ambayo ni mhimili wa ubinadam. Utashiriki katika mapambano haya katika hali ya usawa ambao utashinikiza mapambano dhidi ya umasikini. Hatutoweza sana kutoa elimu, hatutoweza kutoa dhahabu au fedha, lakini tuna kitu tofauti ambacho hakuna hata mmoja aliyenacho na ambacho wanahitaji kujua – uzoefu wetu wa kuwa watengwa.*

*Tunajua uhuru gani ni bora zaidi kuliko mtu yeyote kwa sababu tulikuwa tukiishi tukiwa ni tegemezi kwa wengine. Tunajua usawa ni bora kwa kiasi gani, kwa sababu tunachukuliwa kama wanyonyaji na binadam walio duni. Tunajua thamani ya kuwa mwanadam, kwa sababu mara zote tumekuwa tukibeba mzigo wa dharau. Tumekwisha pitia hayo yote yanayo mfedhehesha mtu, familia, majirani, na kama tukiungana katika mapambano mengine, itakuwa ni kuwafanya wapambanaji waelewe kuwa kuna watu walio katika tabu zilizokithiri na walio kata tamaa.*

**Bila juhudi zetu, bila ya kujitolea kwetu, maisha bora hayatakuja kwa muujiza**
(ushuhuda wa Hassan Abeid)




Kwa mimi, ujumbe uliosomwa ni changamoto ya kuendeleza juhudi zetu katika maisha magumu tunayo kwenda nayo.

Kitu cha kwanza muhimu ni kwamba hali ngumu za maisha zitambuliwe na hao ambao wana uwezo zaidi. Tunahitaji kufanya juhudi kwa ajili ya kuwaeleza kuwa hatuikubali hali yetu ngumu ya maisha. Kupitia uzoefu wetu katika maisha, tunaweza kubadilisha fikra na dhana za hao ambao wana maisha bora, kuwaonyesha jinsi tunavyo pambana na umasikini uliokithiri. Nafikiri kwamba, tunatakiwa kushiriki na kushirikiana na wajumbe wa ATD, kusimama na kutetea haki zetu kama ; elimu bora kwa watoto wetu, huduma bora za afya n.k. Tunataka utu wetu utambuliwe, tunata kuheshimiwa kama wanadamu, tunataka kupata haki sawa bila kuhukumu muonekano wetu. Yote haya yanawezekana.

Kitu cha pili muhimu, katika ujumbe huu uliosomwa ni kwamba tunatakiwa pia kuwa tayari kubadili fikra zetu, mawazo yetu. Uzoefu wetu unatokana na mazingira tunamoishi, lakini tunatakiwa kuwa tayari kusongambele kuyaelekea maisha bora ya baadaye.

Kila mara hukaa pamoja, hutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kupanua mawazo yetu, kushirikishana uzoefu wetu na kwa kugundua njia mpya za kupambana na umasikini uliokithiri. Sasa ni muda wetu kukumbushana kuwa bila juhudi zetu, bila ya kujitolea kwetu, maisha bora hayatakuja kwa muujiza.

Tunatakiwa tayari kujifunza na kusaidiana katika kujifunza kusoma na kuandika. Kwa hiyo ninajaribu kutumia muda wa mapumziko kwa ajili ya kuwasaidia wenzangu wanaojifunza kusoma na kuandika Kiswahili kwa sasa.

Kitu cha tatu muhimu katika ujumbe huu uliosomwa ni kwamba sisi ambao tunaishi katika hali ngumu, tunatakiwa kuwa katika mshikamano kwa ajili ya kuunda umoja katika maeneo tunamo ishi na maeneo ya kazi.

Katika Soko la samaki, ikiwa mmoja wa wenzetu anapopata tatizo ambalo ni zito sana kujiokoa nalo kama ugonjwa kwa mfano, tunachangia kwa kumpa msaada na wakati mwingine tunampeleka hospitali kupata matibabu. Tunasaidiana bila kujali dini au muonekano. Hatufurahii kuishi katika mazingira magumu sana. Tunapokuwa katika umoja, tunaweza kuwafanya watu kuwa na maisha bora.

Ningependa nimalizie kwa ushauri : Mabibi na Mabwana, kila mmoja anatakiwa ajisikie wa kwanza kutoa hisi zake kutokana na maelezo haya na kuzionyesha kwa kuchukua hatua.

## Kama mzazi, sitojibweteka

(ushuhuda wa Pachaka ulisomwa na Saasita)




Naitwa Pachaka, ni mchunzi katika Soko la samaki. Nina watoto watatu na nafikiri kuwa kitu muhimu kabisa kama mzazi ni kuwapenda watoto na kuwapa elimu bora, kama inawezekana hata mpaka elimu ya juu.

Sikupata elimu kwa sababu nilikuwa mvivu nilipokuwa mtoto, na niliacha shule nikiwa darasa la pili. Kwa kutokuwa nimeelimika, sijui mambo mengi kuhusu hii dunia. Ninaishi bila ya mwangaza. Mara nyingi kazi ni kwa watu walioelimika na si kwako kwa sababu hujui kusoma na kuandika. Ndio maana nimeamua kujifunza kusoma na kuandika. Ni lengo langu kupata mwanga huu.

Ningalipenda kuwa na uhakika kuwa watoto wangu wanapata elimu bora ili wawe na maisha mazuri kuliko ya kwangu hivi sasa.

Najivunia kuwa mwenye nguvu na afya, bado kijana kwa hiyo ninauwezo wa kubadilisha maisha ya familia yangu. Sitopoteza tumaini langu. Kama mzazi, sitojibweteka. Maisha mazuri ya baadae ya watoto wangu, yamo mikononi mwangu.



## Tunatakiwa tuwapeleke katika vituo vya ufundi ili wapate ujuzi na kujifunza kazi

(ushuhuda wa Ummi na Zainab ulisomwa na Happy)

Sisi ni Ummi na Zainab, mama wawili tunaofanya kazi kama wauzaji wa kuni katika Soko la samaki. Sisi sote tunafikiri kuwa tunawajibika kufanya tuwezavyo kwa ajili ya kuwapatia elimu bora watoto wetu. Kwa mfano, tuko karibu kabisa na walimu wa watoto wetu na huwa tunakutana nao mara kwa mara. Pia, kila baada ya siku tatu au nne hutumia muda kukagua masomo yao. Ni faraja kwao na ni muhimu kujua kama kila kitu kina kwenda vizuri au kama wanahitaji msaada. Mwaka uliopita, mtoto wangu wa kike hakuwa akijua kusoma akiwa darasa la tatu. Niliamua kumlipia masomo ya ziada baada ya shule, nililipia shillingi 10.000 kwa mwezi na ilikuwa msaada mzuri kwake, sasa anaweza kuhesabu, anajua kusoma na anamwandiko mzuri. Maendeleo ya watoto hutegemea zaidi usimamizi wa wazazi. Kwa sababu ya kazi zetu, tunatoka mapema mno na kurudi tukiwa tumechelewa sana. Ni muhimu kujua kuwa majirani wanakubali kuwaangalia watoto wetu na kuwakumbusha wasisahau kazi zao za nyumbani. Tunaweza kusaidiana kwa njia tofauti tofauti. Watoto wetu wanapomaliza elimu ya msingi, tunatakiwa tuwapeleke katika vituo vya ufundi ili wapate ujuzi na kujifunza kazi. Kuhusu umasikini, tunaweza kupata mawazo kutoka kwa watu wengine na kuweza kupanua fikra zetu. Tunaweza kujifunza mambo mengi kwa kushirikishana na wengine.

## Urithi pekee nitakaoweza kumpa ni elimu

(ushuhuda wa Selemani ulisomwa na Shabani)



Naitwa Selemani na nafanya kazi kama mchuuzi wa Pweza katika Soko la samaki. Natokea katika familia masikini sana. Niliwapoteza wazazi wangu nilipakuwa mdogo na makuzi yangu yalikuwa ni magumu sana. Sasa nina mtoto wa miaka mitatu na kwa sababu maisha ni magumu, najua kuwa urithi pekee nitakaoweza kumpa ni elimu.

Hata hivyo, nchi yetu ni kama kijiji kilicholala : hakuna shule za umma kwa watoto wa miaka mitatu. Watoto wangu hubaki nyumbani tu, kwa sababu wazazi kama mimi hatuna uwezo wa kuwalipia ada kwa shule za binafsi.

Ili kuhakikisha kuwa mtoto wangu ataweza kuendelea na shule hata kama naweza kuwa na matatizo hapo baadaye. Ningependa kufungua akaunti benki na kuweka fedha kidogo kidogo mara kwa mara. Unapojifunza, unaelewa vitu vingi. Elimu haina mwisho.



## Ninacho kifanya ni kwa ajili ya imani yangu tu, na si kwa sababu ya pesa

(ushuhuda wa Shabani)

Jina langu ni Shabani na ninafanyakazi katika machimbo ya mawe Kunduchi. Ningalipenda kuwaambia hisia zangu kuhusu haya maandishi yamesomwa hivi punde na kisha kila mmoja wetu amekaribishwa kujitoa ili kukomesha Umaskini.

Binafsi nimekuwa sehemu ya ATD Dunia ya Nne kwa miaka mingi na tunakutana mara kwa mara kutafakari kuhusu vipaumbele na shughuli za ATD katika Dar es Salaam na maeneo yanayozunguka. Tangia Januari, mwaka huu, najaribu kuzifahamisha familia kadha za kitongoji changu kuwa tunaweza kuja pamoja ili tufanye utaratibu wa kuwapatia watoto wetu vyeti vya kuzaliwa.

Ni vigumu sana kwangu kwa sababu baadhi ya hawa wazazi uniuliza : Kwanini umevutiwa katika suala hili ? Je unapata nini kutokana na kufanya hivi ? Hatutopata chochote, ispokuwa wewe, unakwenda kulipwa pesa kwa kutuhamasisha sisi.

Nawafahamisha kuwa ninacho kifanya ni kwa ajili ya imani yangu tu, na si kwa sababu ya pesa.

Hatahivyo, wanakataa hawaniamini na wanafikiria kuwa nawadanganya. Wakati mwingine ninakatishwa tama kidogo, si tu kwa sababu ya kutopata pesa katika hali ya kujitoa, badala yake upoteza pesa pale ninapoacha kazi zangu ili kukutana na watu au kushiriki katika mikutano ya kazi na hakukuna mtu yoyote anaeniamini. Nataka kuendelea kujitoa na nina uhakika kuwa mkusanyiko kama huu utanisaidia kufanya bayana nini dhamira ya kujihusisha kwangu.

Na washiriki wengine wengi walitoa mawazo yao ya papo kwa papo.















## *Kampeni yetu – miradi miwili ipo katika mchakato*

Kwa sehemu ya pili ya sherehe hii, tutakwenda kushiriki pamoja kuhusu uzoefu halisi wa aina mbili. Miradi hii miwili ipo katika mchakato, mmoja hapo Kunduchi, mwingine katika Soko la samaki. Kunduchi tunawaunganisha pamoja kwa ajili ya kupata vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wetu ; katika Soko la samaki tunafanya kazi pamoja na kusaidiana kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili.

Kama mnavyojua, kila mahali duniani kote, watu hukataa udhalimu na kutaka kubadili maisha ya baadaye ya watoto wao. Tunafikiri kuwa ni muhimu kuwa na ufahamu kwamba, hatuko pekeetu katika dhamira yetu na kuanza kuchukua hatua. Ndiyo maana tunakwenda kuanza kwa kusoma ushuhuda kutoka Bangui, makao makuu ya Jamhuri ya Afrika ya kati. Inaonyesha jinsi wazazi wanavyokutana na ugumu katika upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa vya watoto wao.

## Bila ya cheti cha kuzaliwa, mtoto hatafika mbali, hataweza kuandaa maisha yake ya baadaye

(ushuhuda wa wazazi wanaoishi Bangui)

Karibu watoto wetu wote hawana vyeti vya kuzaliwa kwa sababu hatukuwa na uwezo wa kwenda kujifungulia hospitalini au kulipia gharama za cheti cha kuzaliwa. Wengi wa watoto wetu hawasajiliwa.

Tunajua bila ya cheti cha kuzaliwa, mtoto hatafika mbali, hataweza kuandaa maisha yake ya baadaye lakini ni ghali kwetu kukipata. Tunapata tabu kwa kutokuweza kufanya hivyo ili waweze kwenda shuleni.

Tunamdanganya mkuu wa shule na huwakubali watoto. Tunadanganya kwa sababu watoto wetu waweze kwenda shule. Hata hivyo haitasaidia hadi mwisho.

Wakati watoto wapo katika darasa la mwisho kwa shule ya msingi, uwongo wetu huwa hautoshi kwa sababu tunatakiwa kutoa nyaraka kikiwemo cheti cha kuzaliwa ili wafaulu mitihani. Tunajua kuhusu vijana wadogo ambao ni hodari lakini walisimamishwa kwenda shule karibu na mwishoni mwa elimu ya msingi kwa sababu hii. (...)

Umasikini uliokithiri hutupelekea sisi wenyewe kuwa katika mgogoro na tunachofikiri na tunachokitaka kwa watoto wetu. (...) Kama wazazi, tumeshindwa kabisa. Tunatakiwa kudhihirisha tunachoweza kufanya kwa pamoja, kuungana, kushirikiana fedha zetu, maarifa yetu, uwezo wetu ili Mungu aliye mbele yetu atupe nguvu kuupinga umasikini uliokithiri na kuleta amani kwa kila mtu.



## Mradi wa usajili wa vizazi katika Kunduchi

(ushuhuda ulisomwa na Andrea)

Hapa Kunduchi, sisi ndio haswa wenye hali sawa na ya wazazi walioko Bangui.




Wengi wetu hatuna vyeti vya kuzaliwa vya watoto wetu. Tunajua kuwa, si hali nzuri kwa siku za usoni, lakini hatukufanya kwa sababu tofauti tofauti : ukosefu wa fedha, ukosefu wa nyaraka, ukosefu wa taarifa kuhusu taratibu, umbali wa mahala pa maombi ya vyeti n.k.

Kwa wiki kadhaa, tulianza kuzungumzia suala hili na majirani, jamaa zetu, wenzetu. Tumegundua kuwa wengi wao yanawahusu na wako tayari kufanya kitu.

Tayari katika jumamosi mbili zilizopita tulikusanyika hapa katika eneo hili ambalo tuko hapa leo kwa ajili ya kushirikishana taarifa mbalimbali, kukusanya nyaraka zinazo hitajika na kusaidiana. Tunasaidiwa na ATD katika mradi huu. Lengo ni kuruhusu kila familia kupata vyeti vya kuzaliwa kwa ajili ya watoto wao kupitia masharti mawili :

Sharti la kwanza ni kusongambele pamoja, kila mmoja akijaribu kusaidia wale ambao kwao ni suala gumu zaidi.



Sharti la pili ni kuunda ushirikiano na uongozi wa serikali za mitaa kwa ajili ya kupata msaada kikamilifu.

Kwa sasa, familia zaidi ya arobaini wamejiunga na mradi. Hatua zitakuwa ni ngumu zaidi au kidogo kutegemeana na hali ya kila familia, na kwakweli tutahitaji kuwa pomoja ili kufanikisha. Lengo si kufanikiwa kwa familia nyingi na kuzikatia tamaa nyingine : tunataka hasa, kwamba kila familia inapata vyeti vya kuzaliwa vya watoto wake na tunatakiwa kuwa pomoja kama akina mama kutoka Bangui walivyosema.



## Mradi wa kufuta ujinga katika Soko la samaki
(ushuhuda wa Mngwali ulisomwa na Mbaraka)

Kwa jina naitwa Mngwali, mimi ni mfanyabiashara ya samaki katika Soko la samaki la Magogoni. Mimi ni sehemu ya kamati inayosimamia mradi wa kufuta ujinga katika Soko la samaki na naweza kukuelezea kuhusu mradi.

Watu wengi sana wanaofanya kazi katika Soko la samaki hawajui kusoma na kuandika kwa Kiswahili. Mwaka iliopita, wazo la kufanya hiki kitu likazaliwa katika kitengo cha wauza kuni.

Mradi ulianza Aprili 2009 na wasomaji kumi na mbili, Mwalimu mmoja na masaa ya masomo yakawa mawili mawili kwa Jumatatu na Ijumaa kila wiki. Kulikuwa na wasaidizi, mmoja kwa kila msomaji, ambaye anawajibika kuwatia moyo na kuwasaidia katika kazi zao za nyumbani.

Mwaka uliopita, nilikuwa ni mmoja wa wasomaji na mwaka huu mimi ni msaidizi. Hakuna ambaye hupata fedha yoyote katika mradi huu isipokuwa mwalimu : kila mtu anajihusisha kwa sababu alishawishika kuwa anawajibika kushirikiana alichojifunza siku moja. Baadhi yetu walikuwa na nafasi ya kujifunza na kusoma walipokuwa wadogo, wengine wangejifunza wakati walipokuwa watu wazima : kwa hali yoyote, tulihisi kuwajibika kusaidia wengine leo ili nao waweze kujifunza.



**Kwa kuhitimisha kama ATD Dunia ya Nne hapa Dar es Salaam, tupo tayari kusaidia hatua mtakazo zichukua katika maeneo hayo mawili**

Kupitia shuhuda hizi mbili kuhusu miradi kwa Kunduchi na katika Soko la samaki, unaweza kuelewa kuwa kama ATD Dunia ya Nne hapa Dar es Salaam, tupo tayari kusaidia hatua mtakazo zichukua katika maeneo hayo mawili : kupata vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wenu na kujifunza kusoma na kuandika kwa ajili yenu wenyewe.

Kuhusu mradi wa usajili wa vizazi hapa Kunduchi, kwanza tunataka kufanikisha tukiwa na familia arobaini kwanza na katika muda wa miezi michache ijayo, tunaweza kuendelea na familia nyingine kutoka Tegeta na maeneo yanayoizunguka. Kando na hayo, tuko tayari kusaidia mradi huu kwa Tandale au katika Soko la samaki kama baadhi yenu mtavutiwa.

Kuhusu mradi wa kufuta ujinga, mnajua kuwa muhula huisha katika kipindi cha miezi sita na huhusisha wasomaji kumi na mbili na wasaidizi kumi na mbili pia. Kama baadhi yenu wako tayari kusimamia mradi wa kufuta ujinga kama wafanyavyo katika Soko la samaki, tuko tayari kuwasaidia. Pengine ni muda mzuri kwenu kuchukua ushauri kutoka kwa wale wanaotokea katika Soko la samaki.

Kuna eneo la tatu ambalo hatukuliongelea leo na ambalo tuko tayari kusaidia katika juhudi zenu : ambalo ni upatikanaji wa elimu ya msingi. Pengine unakumbuka kuwa tulizungumzia kuhusu hili mwaka uliopita tulipokuwa tukisherehekea Mei 15.



## *Hitimisho*

Sasa ni muda wa kuhitimisha sherehe hii ya kimataifa ya familia kwa mwaka 2010.

Wakati wazazi wakiongea na wengine wakisikiliza, watoto walitengeneza michoro na kuandika ujumbe kwa watoto walioko Kongo na kukabidhi kwa Justin, Jules na Papa Emile.











Kabla ya kufunga mkutano huu napendekeza msikilize ujumbe huu wa mwisho kutoka katika baadhi ya ***familia za Burkina Faso***.

*“Watoto wetu ndio tumaini letu la baadaye. Muhimu zaidi ni mafanikio ya watoto wetu. Kama mtoto anafanikiwa, atakuwa ni mtoto wa kila mtu, lakini kama atafeli kila mtu atamkataa. Maombi haya yako mioyoni mwa akina mama wote.*

*Watoto wetu wanahitaji kujua magumu yetu na hili itawapa ujasiri kusoma na kufanikiwa katika maisha. Ikuwa ni msaada wa kutokuwa na maisha magumu kama tuliyonayo sisi wenyewe. Watoto wanahitaji kujipenda na kuwa ni wenye kujiamini. Wao ni tumaini letu la baadaye.*

*Mtoto ni wa thamani, tungependa kwamba jamii, uongozi mbalimbali kujivunia kuwa imewekeza kwa maisha ya baadaye ya watoto wote.”*

